



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA
CHUO CHA TAIFA CHA HALI YA HEWA
S.L.P 301
KIGOMA



Simu: : + 255 (0) 28 298 8148

Nukushi: + 255 (0) 28 298 8149

Barua pepe: nmtc@meteo.go.tz

Tovuti: www.meteo.go.tz

(Kimepewa Ithibati Kamili na NACTE kwa No. REG/EOS/025)

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO KWA NGAZI YA
CHETI NA DIPLOMA KATIKA MWAKA WA MASOMO
2018/2019**

Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa ni chuo cha serikali chini ya **Mamlaka ya Hali ya Hewa**, kina uzoefu wa zaidi ya miaka arobaini (40) katika kufundisha wataalamu wa Hali ya Hewa.

Chuo kimepewa ithibati kamili na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Diploma (NTA level 5 & 6) katika mfumo wa umahili (CBET).

Chuo kinakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba kusoma Cheti na Diploma katika Taaluma ya Hali ya Hewa kwa mwaka wa masomo 2018/2019.

SIFA ZA KUJIUNGA

- CHETI (Technician Certificate in Meteorology, NTA Level 5); Mwaka mmoja.**
Mwombaji awe amemaliza kidato cha sita (Form VI PCM/ PGM) na awe amefaulu masomo ya Fizikia na Hisabati katika kiwango cha ufaulu wa "Principal Pass" na zaidi kwa masomo yote mawili; au "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja.
- DIPLOMA (Ordinary Diploma in Meteorology, NTA Level 6); Miaka miwili.**
Mwombaji awe na Cheti cha Hali ya Hewa (Technician Certificate in Meteorology, NTA level 5)

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wote wenye sifa wanaweza kutuma maombi yao kwa *kuandika barua au kujaza fomu ya maombi* inayopatikana katika tovuti www.meteo.go.tz na kuituma kwa Mkuu wa Chuo.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 25/8/2018 saa 9:30 alasiri.

Masomo kwa mwaka wa masomo 2018/2019 yataanza Oktoba 2018.

Waombaji watakaofanikiwa kupata nafasi watajulishwa katikati ya mwezi wa 9, 2018.

NB:

Maombi yote yaambatanishe kivuli cha cheti cha kidato cha 4 & 6 au NTA Level 5, cheti cha kuzaliwa na hati halisi ya malipo ya benki (Bank Paying Slip) kiasi cha Tshs. 10,000/= ikiwa na jina la mwombaji na ilipwe katika benki ya NMB kwa "Account Number" **20101000013** yenye Jina **"DIRECTOR GENERAL, TANZANIA METEOROLOGICAL AGENCY"**

Barua au fomu zote za maombi zitumwe kwa:

**Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Taifa Hali ya Hewa,
S. L. P 301,
Kigoma-Tanzania.**

Kwa mawasiliano: +255 754 452 444 – Mkuu wa Chuo